

Muundo na dhima ya vielezi katika kiswahili
Mussa Omari Amanzi
M.A (Kiswahili)
Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Intitute of Kiswahili, 2016

Tasinifu hii ni Matokeo ya utafiti ulioshughulikia muundo na dhima ya vielezi katika Kiswahili na imegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia tatizo la utafiti na kiunzi cha nadharia kilichotumika katika uchambuzi wa mada. Sura ya pili imefanya mapitio ya maandiko mbalimbali yaliyoibua utafiti huu. Sura ya tatu imefafanua mbinu anuwai zilizotumika kuendesha utafiti huu, sura ya nne imejijhusisha na uchanganuzi wa data ulioibua mchango mpya wa utafiti huu ambapo sura ya mwisho imefunga mjadala kwa kutoa muhtasari wa tasini nzi na ushauri kwa utafiti mwingine unaonekana na utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, kimofolojia, vielezi vya Kiswahili vinaweza kuundwa kwa kuongeza (ki-) mwanzoni mwa baadhi ya nomino au vivumishi; kuongeza (ku-) mwanzoni mwa baadhi ya vimilikishi; kuongeza (vi-) mwanzoni mwa baadhi ya vivumishi; kuongeza kiangami (-ni) mwishoni mwa baadhi ya nomino za muelekeo na baadhi ya maneno yasiyo na kategoria yoyote (vielezi asilia/ushadidi). Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa kisintaksia, baadhi ya mafungu ya maneno hufanya kazi za uelezi kamavile kirai elezi ambacho kinaweza kuundwa na kielezi peke yake; kielezi zaidi ya kimoja; mfano E + E, (anakula vizuri sana), E + E + E, (anampiga paka sokoni asubuhi mapema); kielezi pamoja na kihusishi E + H, (anachuma maua juu ya mti) E + E + H, (anafundisha somo vizuri sana mbele ya darasa); kirai husishi elezi (anacheza mpira kwa madaha), pia, kishazi elezi ambacho huundwa kwa kuanza na maneno ya viunganishi vinavyounganisha sentensi zaidi ya moja ndani ya sentensi moja, ambavyo vinachanua utegemezi (kishazi tegemezi), kama vile japokuwa, ingawa kwa sababu kama na mengine mengi; mfano (juma anakula chakula, ingawa anaumwa tumbo), si hivyo tu, bali kisintaksia, utafiti umeonesha namna ya utokeaji wa vielezi katika tungo za Kiswahili kwa vielezi kuhamahama kwa kuwa mwanzo, kati au mwisho; (N + T+E) N+T+E+N)(E+N+T+N) kuhamahama huku kunategemea zaidi kama vielezi vinaelezea neon tu au sentensi nzima au yambwa lakini hutokea kukaa karibu na kijalizo chake (antecedent) na wakati mwingine hukubali kukaa mwanzoni mwa tungo. Matokeo ya utafiti huu yameonesha pia, kisemantiki, vielezi vina dhima mbalimbali katika tungo za Kiswahili. Dhima kuu ya vielezi ni kueleza zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi, kielezina sentensi nzima kwa kukumisha umahali, uwakati, uidadi na unamna. Pia, utafiti umeeleza maana mahususi zinazojitokeza wakati vielezi vinapohamama kwa kuwa mwanzo, kati au mwisho. Kwa ujumla, vielezi katika lugha ya Kiswahili vina miundo yake maalumu na dhima zinazojipambanua katika lugha ya Kiswahili tu.